

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA AROBAINI NA NANE**

**09 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA NANE – TAREHE 09 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

396. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE  
(TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kituo cha Afya Upuge kinahitaji jengo kwa ajili ya Mashine za Mionzi yaani X-ray na *Ultrasound*:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya mashine hizo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**397. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

- (a) Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na wizi wa vyuma unaosababishwa na kushamiri kwa biashara ya chuma chakavu nchini;
- (b) Je, Serikali haioni kwamba biashara ya vyuma chakavu ni hatarishi hata kwa usalama wa raia na mali zao.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**398. MHESHIMIWA ABDALLA RASHID RASHID (KIWANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Jimbo la Kiwani ili kuepusha Wananchi kufuata huduma za Kipolisi kwa umbali mrefu.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **399. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Kilimo Mkataba kwa njia ya *Outgrower Scheme* ili kupanua wigo wa upatikanaji wa Masoko kwa Wakulima wadogo.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **400. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa Uwanja mpya wa Ndege katika Mji wa Njombe utaanza.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **401. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-



Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji wa Kintinku – Lusilile.

**WIZARA YA NISHATI:**

**402. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha kazi ya kupeleka Umeme katika Vijiji 49 vya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ambavyo bado havijapatiwa Umeme.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**403. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Wavuvi wa Ziwa Tanganyika wavue kisasa ili kupata kipato zaidi na kutoa ajira kwa Vijana.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**404. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO  
(BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

- Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha kusindika Chumvi katika Kata ya Ilindi Wilayani Bahi kitakachosaidia kuongeza Mapato ya Halmashauri na kutoa ajira kwa
- Wananchi hasa Akina Mama.



**DODOMA  
09 JUNI, 2021**

**N.J.MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**